أحكام الصيام - سواحيلي

# HUKMU ZA FUNGA




جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# HUKUMU ZA FUNGA

# أحكام الصيام - سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# HUKMU ZA FUNGA.

## أحكام الصيام

Hukumu ya swaumu:
Swaumu ya mwezi wa Ramadhan ni nguzo katika nguzo za uislamu tano, kwa kauli yake Mtume (saw):

((بني الإسلام على خمس: شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمدا رسول الله، وإقام الصلاة، وإيتاء الزكاة، والحج، وصوم رمضان)) [متفق عليه: ٨، ١٦] .

(Uislamu uwejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudulia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa mwenyezi

mungu, na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni mtume wa mwenyezi mungu, kusimamisha swala tano, kutoa zakat, kuhiji na kufunga mwezi wa Ramadhan.) (ameipokea Bukhar na Muslim :8, 16).

Maana yay a swaumu ni kujizuia na kula, kunywa, kufanya tendo la ndoa, na vyote vyenye kufunguza kuanzia kuchomoza kwa alfajir mpaka kuzama kwa jua kwa nia ya kujikurubisha kwa Allah (sw).

Swaumu ya ramadhani ni wajibu Allah anasema:

قوله تعالى: ﴿ فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ﴾ [البقرة:١٨٥] .

(Yeyote mwenye kuushudia mwezi hali ya kiuwa sio mgonjwa wala msafiri basi aufunge) (Al-Baqara: 185).

Kufunga ni wajibu kwa kila muislamu aliefikia baleghe mwenye akili timamu, na baleghe inapatikana pale kijana anapofikia miaka kumi na tano na kuota nywele za sehemu za siri, aukutokwa na manii kwa kuota au kwa namna nyingine, na inazidi kwa mwanamke kwa kutokwa na

hedhi, anapata mtu moja ya vitu hivi basi amebaleghe.

## UBORA WA MWEZI WA RAMADHAN.

Mwenyezi mungu ameuteua mwezi wa ramadhan kuwa ni mwezi wenye fadhila nyingi kulikoni miezi mingine kutokana na nyakati zake, miongoni mwa fadhila zake;

1. Kwamba malaika wanawaombea wenye kufunga msamaha mpaka wafungue.
2. Wanafungwa mashetani waovu.
3. Ndani ya mwezi Ramadhani kuna usiku wa Laylatul Qadir

ambao ni bora kuliko miezi elfu moja.

4. Wanapata msamaha wenye kufunga kila mwisho wa usiku wa Ramadhan.

5. Allah anawaachia huru na moto kila usiku wa ramadhan.

6. Kwamba kufanya umrah ndani ya mwezi wa Ramadhan ni sawa na kufanya Hija.

Na miongoni mwa yale yaliyopokewa kutokana na ubora wa mwezi wa Ramadhan ni Hadithi aliyoipokea Abu Huraira (R.A) anasema, Amesema Mtume (saw):

قال رسول الله ﷺ: (( من صام رمضان إيمانًا واحتسابًا ، غُفر له ما تقدم من ذنبه )) [متفق عليه: ٣٨ ، ٧٦٠].

(Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani hali ya kuwa ana Imaani na kutarajia thawabu, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 38, 760).

Mtume (saw) anasema kuhusu swaumu:

((كل عمل ابن آدم يضاعف الحسنة عشر أمثالها إلى سبعمائة ضعف، قال الله عز

وجل: إلا الصوم فإنه لي وأنا أجزي به ...))

[متفق عليه: ٥٩٢٧، ١١٥١].

(Kila matendo afanyayo mwanadamu yatazidishwa mara dufu, jema moja kwa thawabu kumi mpaka mia saba. mwenyezi mungu anasema: Isipokuwa swaumu, kwani hakika ya swaumu ni yangu na mimi ndie nitaeilipa) (Ameipokea Bukhar na Muslim:5927, 1151).

# KUTHIBITI KUINGIA MWEZI WA RAMADHAN.

Kuthibiti kuingia mwezi wa Ramadhan ni moja kati ya haya mambo yafuatayo;

1. Kuonekana kwa mwezi wa Ramadhan, ukionekanwa mwezi basi ni wajibu kufunga. Mtume (saw) anasema:

قال رسول الله ﷺ : (( إذا رأيتم الهلال فصوموا، وإذا رأيتموه فأفطروا )) [متفق عليه: ١٩٠٠، ١٠٨٠]

(Mtakapouona mwezi fungeni, na mnapouona fungueni) (Amaeipokea Bukhar na Muslim:1900, 1080).

Inatosha kuthibitisha kuonekana kwa mwezi wa Ramadhan mtu mmoja muadilifu, ama kuokana kwa mwezi wa shawwal kwa ajili ya kufungua ni kushuhudia watu wawili waadilifu.

2. Kukamilika kwa mwezi wa Sha'aban siku thelathini, itakapokamilika siku ya thelathini na moja basi hiyo ndio siku ya kwanza ya mwezi wa Ramadhan. Mtume (saw) anasema:

(... فإن غُمَّ عليكم فأكملوا العدة ثلاثين )

[متفق عليه: ١٩٠٧ ، ١٠٨١].

(Utakapozibwa kwenu na mawingu msiuone, basi kamilisheni hesabu ya siku thelathini za mwezi wa Sha’aban)

## WALIORUHUSIWA KULA MWEZI WA RAMADHAN. (KUFUNGUA).

1. Mgonjwa ambae anatarajiwa kupona ikawa ni tabu kwake kufunga, yeye anaruhusiwa kufungua, kisha atailipa zile siku alizofungua siku nyingine, ikiwa mtu ana maradhi endelevu atarajiwi kupona, haimlazimu kufunga, lakini atalisha kila siku masikini mmoja kilo moja na nusu

ya mchele au mfano wake au atapika chakula atamuita masikini aje kula kwa idadi ya siku alizofungua.

2. Msafiri: Inafaa msafiri kufungua mwanzo wa safari yake kutoka mji anaishi mpaka ataporudi ikiwa hajatia nia ya kuishi huko alikokwenda.

3. Inafaa kwa mwanamke akiwa na mimba au kunyonyesha atakapo ogopea nafsi yake motto wake atafungua, ukiondoka udhuru atazikidhi zile siku alizofungua.

4. Mtu mzima (Mzee) ambaye ni tabu kufunga, anaruhusiwa kufungua bila ya kuzikidhi siku

zilizompita, lakini atalisha kila siku masikini.

## VITU VYENYE KUHARIBU SWAUMU.

1. Kula na kunywa kwa akusudi, au atakapokula kwa kusahau swaumu yake haitaharibika, kwa kauli yake mtume aliposema:

لقوله ﷺ : ((من نسي وهو صائم ؛ فأكل أو شرب فليتم صومه...)) [رواه مسلم:١١٥٥]

(Yeyote mwenye kusahau akala au akanywa hali ya kuwa amefunga,

basi aikamilishe Swaumu yake….) (Ameipokea Imamu Muslim :1155).

Katika vitu vinavyofunguza pia ni kufikisha maji kwenye koo kwa kutumia njia ya pua, au kupitisha chakula katika njia ya mshipa, au kuongewa damu, vyote hivyo vinaharibu swaumu ya mfungaji.

2. Kufanya tendo la ndoa : Wakati akifanya tendo la ndoa mwenye kufunga swaumu yake inaharibika, itamuwajibikia kuikidhi pamoja na kafara ambayo ni kumuacha mtunwa huru, akimkosa atafunga miezi miwili yenye kufuatana hatafungua isipokuwa kwa udhuru wa kisheria, kama vile za

kusherehekea Eid mbili au siku za Tashreek za kuchinja, au udhuru wa kuumwa, kusafiri sio kwa kusudia kufungua.

Ikiwa atafungua bila ya udhuru hata kama ni siku moja itamlazimu kuanza upya kufunga ili ipatikane neno kufuatana, ikiwa atashindwa kufunga miezi miwili yenye kufuatana, basi alishe masikini sitini.

3. Kujitoa manii kwa khiyari kwa sababu ya kupiga busu, au kujitoa kwa njia ya mkono au njia nyingineyo, kufanya hivyo ni kuharibu swaumu itamujibikia kukidhi siku ambazo alifanya hivyo

bila ya kutoa kafara, ama kuota na kutokwqa na manii mchana wa Ramadhani hakuharibu swaumu.

4. Kutoa damu kwa kupiga hijama au kwa kujitolea damu kusaidia kunaharibu funga, ikiwa atatoa damu chache kwa ajili ya uchunguzi hiyo haiharibu swaumu, vile vile kutoka damu bila ya khiyari kama vile damu za pua, au jeraha, au kung'oa jino hiyo haiharibu swaumu.

5. Kujitapisha kwa makusudi ama kutapika bila ya kukusudia hakuharibu swaumu.

Ikiwa atafanya vitu hivi na hali ya kuwa elewa na kujua basi swaumu

yake itaharibika, lakini ikiwa atafanya kwa kusahau swaumu yake haitaharibika.
Ikiwa atakula kwa kutenzwa kwa nguvu swaumu ni sahihi na wala hatailipa.

6. Kutokwa na damu ya hedhi au Nifasi, muda atakapoona mwanamke damu akiwa amefunga swaumu yake anaharibika, kama inavyokuwa kwa mwanamke ni haramu akiwa hedhi au nifasi kufunga na ni juu lake kuzilipa siku ambazo alifungua.

# VITU AMBAVYO HAVIHARIBU FUNGA.

1. Kuoga au kuogelea na kupata baridi kwa kujimwagia maji kutokana na joto.

2. Kula, kunywa, kufanya tendo la ndoa usiku mpaka kuingia kwa alfajir.

3. Kupiga mswaki mchana wa mwezi wa Ramadhan, bali inapendeza zaidi.

4. Kujitibu kwa dawa za halali isiwe dawa hiyo ni aina ya chakula, inafaa kuchoma sindano isiyo ya chakula, kuweka dawa ya jicho, dawa ya sikiohata kama

kutapatikana aina ya utamu kwenye koo, ikiwa atachelewesha mpaka mwisho wa kufungua ni bora zaidi, lakini inafaa pia kutumia kifaa cha kuvuta katika kufungua mapafu kwa wenye Athma, haifunguzi kuonja kidogo chakula lakini kisifike kwenye koo, hakuna tatizo kusukutuwa na kuingiza maji puani bila ya kupitiliza zaidi yasije yakaingia kooni na pia inafaa kutumia mafuta uzuri au kunusa mafuta uzuri.

5. Mwenye hedhi na Nifasi ikakatika damu wakati wa usiku inafaa kwao kuchewesha kuoga

mpaka kuchomoza kwa alfajirn na hivyo hivyo mwenye janaba.

## UZINDUZI.

1. Atakaposilimu kafiri wakati wa mchana wa Ramadhan ni wajibu kwa kujizuia siku yake yote wala hatailipa siku hiyo.

2. Hapana budi kwa mwenye kufunga kutia nia ya swaumu muda wowote usiku kabla ya kuchoza alfajir kwa swaumu ya faradhi, kwa swaumu nyingine kama vile swaumu ya siku sita za shawwal, swaumu ya arafa, swaumu ya ashura, ama swaumu za sunnah tu kama vile swaumu za siku tatu kila

mwezi, anafaa kutia nia baada ya kuchomoza alfajir na hata kama jua litakuwa limechomoza na kupanda juu kiasi cha mkuki kwa sharti ya kuwa mtu hajakula.

3. Inapekezwa kuwa mwenye kufunga aombe dua wakati akiwa anafungua kwa kile alichokipenda kufungulia, Mtume (saw) anasema:

لقوله ﷺ : (( إن للصائم عند فطره لدعوة ما ترد )) [رواه ابن ماجه: ١٧٤٣]

(Kwa hakika mwenye kufunga ana dua akiomba hairudi inakubaliwa) (Ameipokea Ibn Majah :1743).

Na miongoni mwa dua zilizokuja kutoka kwa mtume (saw) ni dua hii:

((ذهب الظمأ وابتلت العروق وثبت الأجر إن

شاء الله)) [أبو داود: ٢٠١٠].

(Kiu kimeondoka na mishipa imelowa na ujira inshaallah umethibiti) (ameipokea Abu Daud: 2010)

4. Kujua kuingia kwa mwezi wa Ramadhani mchana wa siku hiyo ni wajibu mtu kujizuia na ni juu yake kuja kulipa.

5. Inapendekezwa kwa yule ambaye analo deni la kulipa basi afanye haraka kulilipa ili ajivue na

dhima, na pia inafaa kuchelewesha, ataweza kufunga mfululizo au kidogo kidogo, haifai kuchelewesha mpaka baada ya Ramadhan nyingine.

## SUNNAH ZA SWAUMU.

1. Ni kula daku mtume (saw) anasema :

لقوله ﷺ : (( تسحروا ؛ فإن في السحور بركة )) [ متفق عليه: ١٩٢٣ - ١٠٩٥]

( Kuleni daku kwani kwenyenkula daku kuna Baraka) (ameipokea Bukhar na Muslim:1923, 1095).

Na katika sunnah ya kula daku nu kuchelesha daku mpaka mwisho wa usiku kwa Hadith ya Mtume (saw) inayosema :

لحديث: ((لا تزال أمتي بخير، ما عجلوا الإفطار وأخروا السحور)) [صحيح الجامع : ٢٨٣٥ ].

(Hautaacha kuwa Ummat wangu kwenye kheri watakapofanya haraka kufungua na kuchelewesha kula daku) (Imepokelewa Sahihi Ja'ami:2835).

2. Kufanya haraka kufungua pindi itakapo hakikiwa kuwa jua limezama, na sunnah ya kufungua ni kufungua na tende ukikosa tende, basi fungua kwa kutumia

maji na ukikosa maji utafungua na chochote kilichokuwa ni wepesi kwako.

3. Kuomba wakati wa kufunga na hasa hasa wakati wa kufungua kwa hadithi ya Mtume (saw) anasema:

لقوله ﷺ : (( ثلاث دعوات مستجابات، دعوة الصائم ، ودعوة المظلوم ، ودعوة المسافر )) [رواه البيهقي وغيره].

(Mtume swalallahu Alayhi wa Salaam anasema: Dua za watu watatu ni zenye kukubaliwa, Dua ya mwenye kufunga, Dua ya

mwenye kudhulumiwa, na Dua ya msafiri) (Ameipokea Albaihaqiy).

Na yale yanayotakikana kwa mfungaji ni kisimamo katika mwezi wa Ramadhani kwa Hadithi ya Mtume (saw) aliposema:

لقوله ﷺ : (( من قام رمضان إيمانًا واحتسابًا ، غُفر له ما تقدم من ذنبه )) [ متفق عليه: ٢٠٠٩ ، ٧٥٩]

(Mwenye kusimama mwezi wa Ramadhan hali ya kuwa ana Imaan na kutarajia malipo kutoka kwa Allah atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia) ( Ameipokea Bukhar na Muslim :2009, 759).

Inatakikana kwa muislamu kukamilisha swala ya tarawehe pamoja na Imamu kwa kauli yake Mtume (saw) aliposema :

((من قام مع إمامه حتى ينصرف كُتِبَ له قيام ليلة )) [رواه أهل السنن].

(Mwenye kusimama pamoja na Imamu wake kisimamo cha Ramadhan mpaka akamaliza ataandikiwa amesimama usiku) (Imepokelewa na Asw-habu sunani).

Na miongoni mwa mambo ambayo yanatakikana mwezi wa Ramadhan ni kutoa swadaka kwa wingi sana.

Kama vile inavyotakiwa kujitahi kusoma Quran kwa wingi kwenye mwezi wa Ramadhan na mwezi wa Ramadhan ni mwezi wa Quran, kwani mwenye kusoma Quran kila herufi moja anapata thawabu kumi na jema moja ni thawabu kumi na mfano wake.

## SWALA YA TARAWEHE.

Tarawehe ni kisimamo cha usiku mwezi wa Ramadhan kusimama jama'a, wakati wake ni baada ya swala ya Ishai mpaka kuchomoza kwa alfajir, kwa hakika Mtume (saw) alitilia mkazo katika kusimama mwezi wa Ramadhan na ni sunnah

kuswali rakaa kumi na moja na kutoa salamu kila baada ya rakaa mbili.

Atakapozidisha zaidi ya hizo rakaa kumi na moja hakuna tatizo, na katika sunnah za swala ya tarawehe kutokufanya haraka na kufanya kisomo kirefu kisichowapa tabu wenye kuswali.

Hakuna tatizo ikiwa watahudhuria kwenye swala ya tarawehe wanawake ikiwa hakuna fitna, kwa sharti la kutoka kwa heshima sio kudhihirisha mapambo yao wala kujipaka manukato.

# SWAUMU ZA SUNNAH.

Mtume swalallahu alayhi wassalaam alipendekeza na kutilia mkazo kufunga siku zifuatazo;

1. Kufunga siku sita za mwezi wa Shawwal kwa kauli yake mtume:

لقوله ﷺ : ((من صام رمضان ، ثم أتبعه ستًا من شوال، كان كصيام الدهر )) [ رواه مسلم: ١١٦٤ ].

(Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani kisha akafuatisha siku sita za mwezi wa Shawwal atakuwa kana kwamba amefunga mwaka mzima) (Ameipokea Imamu Muslim: 1164).

2. Swaumu ya siku ya jumatatu na Alhamisi.

3. Swaumu ya Siku tatu za kila mwezi akifunga siku ya masiku meupe ni bora zaidi nazo ni tarehe 13, 14 na 15 ya kila mwezi kalenda ya Hijriya sio ya miladiya.

4. Kufunga siku ya Ashurah ambayo ni tarehe kumi ya mwezi wa Muharam, na inapendekezwa kufunga siku moja kabla yake au siku moja baada yake kuwakhalifu mayahudi.

قال رسول الله ﷺ : (( صيام يوم عاشوراء ، أحتسب على الله أن يكفر السنة التي قبله ))

[ رواه مسلم: ١١٦٢ ].

Mtume (saw) anasema katika hadithi aliyoipokea Abu Qatada (R.A) kuwa : (Swaumu ya siku A'shura natarajia kwa Allah ujira wa malipo ya kusafutiwa madhambi ya mwaka uliopota) (Ameipokea Imamu Muslim:1162).

5. Swaumu ya siku ya A'rafa nayo ni siku ya tisa ya mwezi wa Dhul-Hija kwa hadithi ya Mtume (saw) inayosema :

لحديث: « صيام يوم عرفة ، أحتسب على الله أن يكفر السنة التي قبله، والسنة التي بعده » [ رواه مسلم: ١١٦٢ ].

((Swaumu ya siku ya A'rafa natarajia malipo ya kufutiwa madhambi ya mwaka kbla yake na mwaka baada yake)) (Amepokea Imamu Muslim 1162).

## SIKU AMBAZO NI HARAMU KUFUNGA.

1. Kufunga siku ya Eid mbili, Eidl fitri na Eidil adh-a.
2. Kufunga siku za Tashriq tatu, tarehe kumi na moja, kumi na mbili

na kumi na tatu katika mwezi wa Dhul –Hija, na anajizua na hili kwa mwenye kuhiji kwa nia ya kuunganisha (kati ya Umrah na Hija) au tamatuu ikiwa hajapata kichinjo.

3. Kufunga za hedhi na nifasi kwa mwanamke.

4. Kufunga sunnah mwanamke na mumewe yupo bila ya idhini yake, kwa kauli ya Mtume (saw) anasema:

لقوله ﷺ : ((لا تصوم المرأة وبعلها شاهد ، إلا بإذنه، غير رمضان)) [متفق عليه: ٥١٩٢ ، ١٠٢٦].

(Asifunga mwanamke swaumu ya sunnah na mume wake yupo

isipokuwa kwa Idhini ila swaumu ya Ramadhan) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 5192 , 1026).

# FIHRISI YA KITABU

HUKMU ZA FUNGA.................................. 3
UBORA WA MWEZI WA RAMADHAN...... 6
KUTHIBITI KUINGIA MWEZI WA RAMADHAN. ......................................... 10
WALIORUHUSIWA KULA MWEZI WA RAMADHAN. (KUFUNGUA). .................. 12
VITU VYENYE KUHARIBU SWAUMU. ..... 14
VITU AMBAVYO HAVIHARIBU FUNGA... 19
UZINDUZI. ............................................ 21
SUNNAH ZA SWAUMU. ......................... 24
SWALA YA TARAWEHE. ........................ 29
SWAUMU ZA SUNNAH. ........................ 31
SIKU AMBAZO NI HARAMU KUFUNGA.. 34